

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**RATIBA YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI
(PRIMARY SCHOOL LEAVING EXAMINATION TIMETABLE)**

SEPTEMBER 2018

TAREHE NA SIKU	MUDA (SAA)	NAMBA MFICHO	SOMO
05.09.2018 JUMATANO	2:00 – 3:30	01	KISWAHILI
	3:30 – 4:30		MAPUMZIKO
	4:30 – 6:30	04 04E	HISABATI MATHEMATICS
	6:30 – 8:30		MAPUMZIKO
	8:30 – 10:00	02	ENGLISH LANGUAGE
<hr/>			
06.09.2018 ALHAMISI	2:00 – 3:30	05 05E	SAYANSI SCIENCE
	3:30 – 4:30		MAPUMZIKO
	4:30 – 6:00	03 03E	MAARIFA YA JAMII SOCIAL STUDIES

MAELEKEZO MUHIMU

1. Hakikisha kuwa unayo **Ratiba ya Mtihani ya mwaka 2018** ilioandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.
2. **Kabla ya kufungua bahasha** yoyote yenyewe maswali ya Mtihani, hakikisha kwamba **unasoma jina la somo juu ya bahasha husika** na kujihakikishia kuwa somo hilo ndilo linalostahili kufanyika wakati huo kulingana na **Ratiba ya Mtihani**.
3. Endapo utata utajitokeza kati ya maelekezo **yaliyomo ndani ya Karatasi ya Mtihani** na **Ratiba ya Mtihani**, maelekezo **yaliyomo katika karatasi ya Mtihani husika ndiyo yatakayofuatwa**.
4. Watahiniwa **WASIOONA** na wale wenye **UONI HAFIFU** waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 10 KWA KILA SAA** kwa Mtihani wa **Kiswahili, English Language, Maarifa ya Jamii na Sayansi**.
5. Watahiniwa **WASIOONA** na wale wenye **UONI HAFIFU** waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 20 KWA KILA SAA** kwa mtihani wa **Hisabati**.
6. Msimamizi wa watahiniwa **WASIOONA** awe mtaalamu mwaminifu aliye na **uwezo wa kusoma maandishi na alama za ‘Braille’**.
7. Watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** wapewe karatasi za mtihani na za kujibia zenyewe **maandishi yaliyokuzwa**, zilizoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa matumizi yao.
8. Karatasi zenyewe majibu ya watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** zifungwe kwenye **bahasha za pekee**. Zisichanganywe na karatasi za watahiniwa wenye Uoni wa kawa.
9. Watahiniwa waelekezwe;
 - (a) Kuingia ndani ya chumba cha mtihani nusu saa kabla ya muda wa mtihani na watakaochelewa kwa zaidi ya nusu saa baada ya mtihani kuanza hawataruhusiwa.
 - (b) Kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na wasimamizi wa mtihani.
 - (c) Kuandika namba ya mtihani kwa usahihi.
 - (d) Kutofanya mawasiliano ya maneno au kwa njia yoyote baina ya watahiniwa. Ikiwa mtahiniwa ana tatizo anatakiwa kunyosha mkono ili kuomba msaada kwa msimamizi wa mtihani.
 - (e) Wakijihuisha katika udanganyifu watafutiwa matokeo yao ya mtihani.